# MISINGI IMARA

## Jenga maisha yako juu ya kazi iliyokamilika ya Kristo

KEN LEGG

*Misingi Imara* na Ken Legg
ISBN: 978-0-9924120-0-5
Kimechapishwa na: Ken Legg Ministreis
P O Box 4185
Elanora Queensland 4221
Australia
ken@kenlegg.com.au
Tovuti:
www.kenlegg.com.au

© Hakimiliki: Ken Legg, 2014. Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kunaswa tena au kusambazwa kwa namna yoyote au kwa njia yoyote, kielektroniki au kimitambo, ikijumuisha kunakili, kurekodi au kwa mfumo wowote wa kuhifadhi na kurejesha taarifa, bila kibali kwa maandishi kutoka kwa mchapishaji.

Kumbuka: Ni kinyume cha sheria na ni ukiukaji wa maadili ya Kikristo kunakili kitabu hiki bila ruhusa kwa maandishi kutoka kwa mchapishaji.

Shukrani:
Isipokuwa ionyeshwe vinginevyo manukuu ya Maandiko katika toelo hili yametoka katika Biblia Takatifu, Swahili Union Version, hakimiliki ya 2005, Chama cha Bibilia Cha Kenya na Chama Cha Bibilia Cha Tanzania. Imetumika kwa ruhusa.

Kimechapishwa Kenya.

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| Somo # 1 | Misingi ya Mitume | 4 |
| Somo #2 | Haki | 8 |
| Somo #3 | Utambulisho | 12 |
| Somo # 4 | Dhamiri Ya haki | 15 |
| Somo # 5 | Neema | 19 |
| Somo # 6 | Imani | 23 |
| Somo # 7 | Agano Jipya | 27 |
| Somo #8 | Wana wa Mungu | 31 |
| Somo # 9 | Kiumbe Kipya | 35 |
| Somo # 10 | Mtu Mpya | 39 |
| Somo # 11 | Upendo wa Mungu | 43 |
| Somo # 12 | Uzima wa Milele | 47 |

# Somo # 1 - Misingi ya Mitume

- ✓ Sehemu muhimu zaidi ya jengo ni sehemu ambayo huwezi kuona - misingi. Ndivyo ilivyo pia kanisani.
- ✓ Misingi huelekeza mipaka na umbo la jengo. Inaashiria kile kinachoweza kujengwa juu yake.
- ✓ Kazi kuu ya mitume ni kuweka misingi. *"Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni."* (Waefeso 2:20).
- ✓ Misingi ni Yesu, 1 Wakorintho 3:11. Mitume waliwafundisha wanafunzi jinsi ya kuwa na mizizi na msingi ndani Yake.
- ✓ Wanafunzi 12 walifunzwa na Yesu kwa miaka 3 kwa ajili ya huduma hii. Mafundisho yao yakajulikana kama Mafundisho ya Mitume, ambayo walipaswa kuweka kama msingi kwa Wakristo na makanisa.

**Paulo Alikuwa Mtume Kwa Mataifa** (Wagalatia.1:11&12)

- ✓ Kama Yesu alivyowafundisha wanafunzi kwa miaka 3, ndivyo alivyomwagiza Paulo kuhusu jinsi kanisa lingejengwa.
- ✓ Kama mkuu wa wajenzi Paulo aliweka misingi ya makanisa ya mashinani, 1 Wakorintho 3:10-11.
- ✓ Alikuwa na mkusanyiko mkubwa wa kweli ambazo alifundisha kwa kina na kwa upana katika makanisa yote.
- ✓ Aliutaja hizi kuwa 'aina ya elimu'. Kwa Warumi aliandika: *'...lakini mliitii kwa mioyo yenu ile <u>namna</u> ya elimu ambayo <u>mliwekwa chini yake</u>."* (Warumi 6:17). Hizi zilikuwa kweli muhimu kwa waumini kujengwa juu yake.
- ✓ Tamko lililotafsiriwa 'mliwekwa chini yake' lina maana ya kukabidhiwa kwa kitu au mtu fulani.
- ✓ Chini ya kila agano watu wa Mungu walikabidhiwa kwa mafundisho ya agano hilo.
- ✓ Musa aliposhuka mlimani akiwa na zile amri 10, Si kwamba alizikabidhi tu kwa Waisraeli, bali pia aliwakabidhi Waisraeli kwa amri hizo.
- ✓ Walikabidhiwa *"namna ya maarifa na ya kweli katika torati."* (Warumi 2:20).
- ✓ Basi msingi wa jinsi Mungu alivyohusiana na watu wa agano la kale

ulikuwa kulingana na torati. Huu ulikuwa umbo au sura ya uhusiano wao na Yeye.

- ✓ Akizungumzia wakati huu, Paulo anasema, *'...tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ije ile imani itakayofunuliwa.'* (Wagalatia 3:23).
- ✓ Lakini tunaposikia na kuamini injili tunakombolewa *kutoka* kwa torati na kukabidhiwa kwa mafundisho ya mtume. Paulo alisema, *"Bali sasa tumefunguliwa katika torati, tumeifia hali ile iliyotupinga,..'* (Warumi.7:6).
- ✓ Aina ya mafundisho ya Paulo imeainishwa katika nusu ya kwanza ya Warumi sura ya 6. Inahusu ubatizo wetu katika kifo cha Kristo, kuzikwa na kufufuka kwake.
- ✓ Hii ndiyo injili (Tazama 1 Wakorinthi 15:1-4). Sio tu kwamba Yesu alisulubishwa, akazikwa na kufufuliwa kwa ajili yetu, lakini sisi pia tulikufa, na kuzikwa na kufufuliwa pamoja naye katika upya wa uzima.
- ✓ Katika muungano huu naye tunawekwa huru kutoka kwa namna ya agano la kale na kukabidhiwa kwa namna ya mafundisho ya mitume ya agano jipya.
- ✓ Tunapoamini mafundisho ya mitume maisha yetu yanajengwa kwayo.
- ✓ Kwa kuunganishwa na Kristo tunashiriki katika ukamilifu wa kifo chake na nguvu ya maisha yake ya ufufuo. Haya ndiyo maisha halisi ya Kikristo.

**Mfano Wa Maneno Ya Uzima**

- ✓ Namna ya mafundisho ya mitume inatengenezwa na *"kielelezo cha mafundisho yenye uzima"*, yaani maneno muhimu yanayohusiana na maisha yetu katika Kristo. Paulo alimwagiza Timotheo: *'Shika kwa uthabiti kielelezo cha mafundisho yenye uzima yale uliyoyasikia kwangu,..'*(2 Timotheo 1:13).
- ✓ Tumemiminwa katika kalibu hii ya maneno yenye uzima.
- ✓ Baadhi ya maneno yenye uzima ya Paulo yalikuwa: haki, katika Kristo, neema, imani, wana wa Mungu, kiumbe kipya, agano jipya, mtu mpya, upendo wa Mungu, uzima wa milele, n.k.
- ✓ Tunaposhika sana maneno haya yenye uzima yanatengeneza maisha yetu.
- ✓ Neno la Kigiriki la 'uzima' linamaanisha afya. Mafundisho yenye afya

husababisha maisha yenye afya.

**Kujengwa Na Maneno Yasiyo Na Uzima Ya Mafundisho Ya Kibinadamu**

✓ Ikiwa hatujaimarishwa katika misingi ya mitume, basi kuna uwezekano mkubwa tumejengwa na namna ya mafundisho ya kibinadamu.

✓ Haya yamejawa na matamshi yanayotumika sana katika duru za kidini ambamo tumetoka.

✓ Kinyume na kielelezo cha mafundisho yenye uzima ambayo Paulo alifundisha, maneno haya yanatilia mkazo nafsi na ni mageni kwa agano jipya.

✓ Kwa hiyo, yanaibua dhana mbovu na zenye kupotosha kuhusu maisha ya Kikristo.

✓ Kwa mfano, matamshi yayotumika katika baadhi ya duru za kidini ni pamoja na: 'kufanya uamuzi au kujitolea', 'kulipa bei', 'kuingia', 'kupenya', 'hatua 4 za…', 'maono', 'kuwa kwenye makali', 'kupanda mbegu ili kupokea mavuno', 'uamsho', ‘kupokezwa’, 'ukombozi', 'kuvunja laana', 'kujitolea' n.k.

**Mkakati Wa Paulo Wa Kujenga Kanisa**

✓ Kwanza angefundisha aina hii ya kweli msingi za mitume kwa watu muhimu kama vile Timotheo na Tito.

✓ Kisha angewaagiza wafundishe viongozi wa mashinani, ili waweze kuwafundisha watu katika makanisa yao.


✓ Kwa mfano, alimwambia Timotheo, *“*Na *mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha wengine vile vile.’* (2 Timotheo 2:2).

✓ Akamwambia Tito, imempasa mzee*, “...akilishika lile neno la imani vile*

*vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga…”* (Tito 1:9).

✓ Ni wazi kwamba wale wanaoongoza, wanaofundisha au kuwashawishi wengine wanapaswa kwanza kujiimarisha wenyewe katika misingi ya mitume. Vinginevyo watakuwa viongozi vipofu wa vipofu.

✓ Uwezo wa kufundisha wengine hauhitaji kuwa katika huduma ya hadharani au ya mimbari, bali wazee wanapaswa kuwa na uwezo wa kusomesha au kuwafunza watu mmoja-mmoja katika misingi imara ya mitume.



**Kwa Majadiliano**

1. Inamaanisha nini, “kuwa na shina na msingi katika Kristo”?

2. Kuunganishwa na Kristo katika kifo, kuzikwa na kufufuka kwake kunamaanisha nini kwako?

3. Ulipookoka, ulikabidhiwa mwanzoni kwa namna ya mafundisho ya mitume au kwa mafundisho ya kibinadamu?

4. Ikiwa ulijengwa na mafundisho ya kibinadamu, ni maneno gani muhimu yaliyotumiwa katika mazingira hayo ambayo sasa unajua kuwa sio ya kibiblia na hata hayafai?

5. 5. Ni muhimu kiasi gani kukombolewa kutoka kwa torati na uhalali wa kidini?

6. Ni maneno gani ya mitume katika orodha iliyo hapo juu ambayo ni yenye thamani zaidi kwako? Je, kuna maneno yoyote katika orodha hii ambayo huelewi? Je, unaweza kufikiria maneno mengine yanayohitaji kujumuishwa kama sehemu ya mafundisho muhimu ya mitume?

7. Jadili nafasi ya Roho Mtakatifu katika ufahamu wetu wa ukweli.

# Somo # 2 - Haki

*"... Wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo..."* (Warumi 5:17).

- ✓ Kupitia zawadi ya haki na wingi wa neema ya Mungu kwetu katika Kristo, tunawezeshwa kutawala maishani.
- ✓ Ikiwa Shetani anaweza kutuzuia ukweli kuhusu *haki* na *neema,* atatuzuia tusipokee kila baraka; kwa sababu tutaamini kwamba ni tabia yetu ndiyo inatustahilisha mambo haya.

Katika somo hili tutaangalia mafundisho ya Agano Jipya kuhusu haki.

**Abrahamu Ni Mfano Wetu**

- ✓ Abrahamu anaitwa *"baba yetu sote"* (Warumi 4:16). Yeye ni kielelezo cha uhusiano wetu na Mungu.
- ✓ Lakini ni kwa njia gani yeye ni kielelezo kwetu? Je, tujaribu kuishi kama alivyoishi?
- ✓ La. Alikosea mambo mengi; lakini alipata jambo la muhimu zaidi! Alikuwa na ufunuo kwamba njia ya Mungu ya haki ni kupitia Yesu.
- ✓ Mungu alimwahidi kwamba kupitia Mzao wake mataifa mengi yangebarikiwa na haki.
- ✓ Alielewa wazi kwamba 'Mzao' ilikuwa inarejelea Kristo. *"Basi ahadi zilinenwa kwa Abrahamu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazawa, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani, Kristo."* (Wagalatia 3:16).
- ✓ Mungu alimhubiria Abrahamu injili! "*Na andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki Mataifa kwa imani, lilimhubiria Abrahamu Habari Njema zamani, kusema, Katika wewe Mataifa yote watabarikiwa."* (Wagalatia 3:8). Yesu akawaambia Wayahudi, "*Abrahamu, baba yenu, alishangilia kwa vile atakavyoiona siku yangu; naye akaiona, akafurahi."* (Yohana 8:56).
- ✓ Abrahamu aliamini injili ile ile tuliyosikia na kuamini.
- ✓ Kwa kuamini habari njema kuhusu Yesu, alifanywa kuwa mwenye haki. *"Abrahamu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki.*

(Wagaltia 4:3). Nasi tu jinsi ile.

**Ubadilishanaji Mkubwa**

Haki ya Mungu ndio msingi wa uhusiano wetu na Mungu. Inatustahilisha kwa kila jambo jema. Inategemea "Ubadilishanaji Mkubwa". *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."* (2 Wakorintho 5:21). Hii inamaanisha:

**A)** **Mungu Anamuhesabia Yesu Dhambi Zetu** (Tazama Warumi 4:7&8)

- ✓ Daudi alifanya dhambi mbili ambazo hungesamehewa chini ya sheria; lakini hazikuhesabiwa kwake.
- ✓ Ingawa Daudi alisimama mbele za Mungu katika dhambi zake, Mungu alimhesabia haki. Mungu, "...*ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa,..*" (Warumi 4:5). Anawezaje kufanya hivyo?
- ✓ Dhambi zetu alihesabiwa Kristo na Yeye alibeba hukumu yake kamili.
- ✓ Katika Mto Yordani, Yesu alitangaza kwamba ubatizo wake ulionyesha kuwa angetimiza haki yote." *Yesu akajibu akamwambia, Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote."* (Mathayo 3:15).
- ✓ Katika ubatizo wake alionyesha kile ambacho kingetokea Msalabani. Angewakilisha jamii ya wenye dhambi, afe kwa ajili ya dhambi zao, azikwe na kuinuliwa tena kama Kichwa cha viumbe vipya ambao ni wenye haki na ambao Mungu anapendezwa nao.
- ✓ Kwa hivyo, hukumu ya dhambi zetu zote - zilizopita, za sasa na zijazo - amehesabiwa Yeye. *"Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo; sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje. Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu."* (Yohana 12:31-32).

**B)** **Mungu Anatuhesabia Haki Ya Kristo** (Tazama Warumi 4:6)

- ✓ Wayahudi hawakujua njia ya Mungu ya haki na walifikiri kwamba wangeweza kuwa wenye haki kwa utiifu wao wa Torati. "*Kwa maana, wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu."* (Warumi 10:3). Wengi hufanya makosa hayo hayo.
- ✓ Hatukufanywa kuwa wenye haki kwa utiifu wetu, bali utiifu wake. *"Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi*

*waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki."* (Warumi 5:19).

- ✓ *Hatutendi* ili kuwa wenye haki; *Tunaamini* na kuwa wenye haki.

**Asiye Na Hatia Au Mwenye Haki?**
Msingi wa baraka ni uhusiano sahihi na Mungu. Adamu alibarikiwa alipokuwa katika uhusiano na Mungu. Lakini alipata laana baada ya kutenda dhambi. Hatumo ndani ya Adamu – watu wasio na hatia hadi wapatikane na hatia. Tumo ndani ya Kristo - wenye haki, hata tunapotenda dhambi.

Kuna tofauti kati ya kutokuwa na hatia na kuwa mwenyehaki:

- ✓ Mtu asiye na hatia afanyapo dhambi, anahesabiwa dhambi yake.
- ✓ Mwenyehaki anapotenda dhambi, dhambi yake imehesabiwa Kristo. Bado amebarikiwa. "*Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi."* (Warumi 4:8).
- ✓ *"... Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao..."* (2 Wakorintho 5:19).
- ✓ *"Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, na dhambi zao sitazikumbuka tena.* (Wahebrania 8:12).


Mfano #1. Mwanzo 12:10-20; 13:1-2. Katika kifungu hiki:

- ✓ Nani alitenda dhambi?
- ✓ Mungu alimkemea nani?
- ✓ Mungu alimbariki nani?

Mfano #2. Mwanzo 20:2-7, 14-16. Katika kifungu hiki:

- ✓ Nani alitenda dhambi?
- ✓ Mungu alionya nani?
- ✓ Nani alibarikiwa?

Mungu alimubariki Abrahamu hata alipotenda dhambi kwa sababu alikuwa mwenye haki kupitia imani katika Kristo. Hii si leseni ya kufanya dhambi. Daima kuna matunda ya dhambi. Lakini Mungu hutubariki kwa msingi wa haki yetu katika Kristo, wala si kwa misingi ya tabia zetu.



**Kwa Majadiliano**

1. Je, kumekuwapo wakati katika maisha yako ya Kikristo ulipoamini kwamba ulikuwa umehitimu au labda hauhitimu kupata baraka na upendeleo wa Mungu kwa misingi ya tabia yako?

2. Je, unaamini kwamba dhambi zako zote - zilizopita, za sasa na zijazo - tayari zimesamehewa?

3. Je, kuna Mkristo yeyote mwenye haki zaidi kuliko Mkristo mwingine?

4. Je, unaweza kusema nini kwa Mkristo ambaye anaamini kwamba haki yake inadumishwa na utiifu wake?

5. Jadili athari za kazi iliyokamilika ya Kristo. Yesu alimaanisha nini aliposema atatimiza haki yote? Na alimaanisha nini alipo paza sauti msalabani nakusema, “Imekwisha!”?

6. Je, habari hii njema inakufanya utake kutenda dhambi zaidi au inakufanya umpende Mungu zaidi?

# Somo # 3 - Utambulisho

Swali muhimu zaidi unaloweza kujiuliza ni, “Mimi ni Nani?”

Cha kusikitisha ni kwamba Wakristo wengi hupokea jumbe za utambulisho wao kutoka kwa vyanzo visivyo sahihi.

Kwa mfano:
- ✓ Mafanikio
- ✓ Kukubalika
- ✓ Mwonekano
- ✓ Tabia

**Wewe Ni Nani?**
Kama Wakristo, hatupokei utambulisho wetu kutokana na mafanikio yetu, tabia au mwonekano wetu, wala kutokana na kukubalika au kutokubalika na wengine.
Utambulisho wetu unategemea yule ambaye tunatambulishwa naye. Warumi 5:12-21 inatuambia:
- ✓ Tulikuwa watu ‘ndani ya Adamu’
- ✓ Sasa sisi ni watu ‘ndani ya Kristo’

Maelezo anayopenda sana Paulo kuhusu Mkristo ni kwamba yeye ni mtu aliye ‘ndani ya Kristo’.

Kuelewa utambulisho wako kama kiumbe kipya ni muhimu kwa afya ya kiroho, kwa sababu, “Si kile tunachofanya ambacho huamua sisi ni nani, bali kujua sisi ni nani ndiko kunaamua kile tunachofanya.”

Ubongo wetu utaelekeza maisha yetu katika mwelekeo wa picha tuliyo nayo kujihusu wenyewe.

Tatizo Wakristo wengi wanapambana nalo ni hili: Wana utambulisho mpya, lakini wamehifadhi mawazo yao ya zamani.

**Kufanya Mabadiliko Kutoka Kwa Fikra Ya Utambulisho Wa Zamani Hadi Fikra Ya Utambulisho Mpya**

Tunafanya mabadiliko kutoka fikra za utambulisho wa zamani hadi fikra za utambulisho mpya kwa kufanya upya fikira zetu.

Katika Warumi 6:1-14, Paulo anashiriki hatua 4 muhimu katika mchakato huu:

1) Warumi 6:3-4 - JUA ya kuwa ulikufa kwa utambulisho wako wa kale katika Adamu na umefufuliwa kiumbe kipya, na utambulisho mpya kabisa katika Kristo.

    ✓ Ukweli ndio unaotuweka huru.
    ✓ Nguvu pekee ya Shetani ni udanganyifu. Anaweza kumtia mtu utumwani kwa kumfanya aamini uwongo.
    ✓ Hatuhitaji kukutana na nguvu; lakini tunahitaji kukutana na ukweli.

2) Warumi 6:8 - AMINI kwamba sasa u kiumbe kipya katika Kristo Yesu.


    ✓ Kujua ukweli haitoshi. Lazima tuamini.
    ✓ Wakristo wengine ni waumini wasioamini!

3) Warumi 6:11 - HESABU kuwa ndivyo ilivyo. Yaani, ishi kulingana na ukweli unaotuhusu sasa.

    ✓ Kuhesabu maana yake ni kufikiria au kukubali ukweli unaotuhusu na kuishi ipasavyo.

4) Warumi 6:13 - VITOE viungo vyako kama vyombo vya kutumikia haki.

    ✓ Mkristo ana asili mpya inayoishi katika mwili wa kale. Mwili tunamoishi ni ule ule tuliokuwa nao kabla hatujaokoka.
    ✓ Hapo awali, tulitii maagizo na matakwa ya mwili; lakini sasa tuko huru kutoka kwa mamlaka ya dhambi.
    ✓ Tunaweza kuchagua kuwasilisha viungo vya miili yetu kama vyombo vya haki.



**Kwa Majadiliano**

1. Je, unapata jumbe za utambulisho wako kutoka wapi?

2. Jadili usemi huu: “Si kile tunachofanya kinachoamua sisi ni nani, lakini kujua sisi ni nani ndiko kunaamua kile tunachofanya.”

3. Je, ni kwa kiwango gani unajua na kuelewa kwamba umekufa kwa utambulisho wako wa kale “ndani ya Adamu” na sasa wewe ni kiumbe kipya ‘ndani ya Kristo’?

4. Ni nini baadhi ya athari za ukweli huu wa ajabu?

5. Kwa nini waumini wengi bado wana mawazo ya kizamani kuhusu utambulisho wao? Ni nini kitakachowasaidia kufanya upya fikira yao kuhusu utambulisho wao wa kiumbe kipya?

6. Jadili hatua 4 katika mchakato wa kufanya upya fikira. Shiriki safari yako katika jambo hili. Uko wapi katika mchakato huu sasa?

# Somo # 4 – Dhamiri ya haki

- ✓ Mwandishi wa Waebrania alisema kwamba hema/hekalu likiwa bado limesimama lilikuwa ni ishara ya ukweli kwamba njia ya kuingia katika uwepo wa Mungu ilikuwa bado haijapatikana (Tazama Waebrania 9:7-8).
- ✓ Ingawa hekalu halisimami tena na njia ya kuingia katika uwepo wa Mungu imefunguliwa, wengi bado hawaifurahii.
- ✓ Pazia la hema ni picha ya kizuizi kinachotuzuia kufurahia uwepo wa Mungu, yaani, dhamiri ya dhambi. *"Huu ulikuwa mfano kwa ajili ya wakati wa sasa, kuonyesha kwamba sadaka na dhabihu zilizokuwa zikitolewa hazikuweza kusafisha dhamiri ya mtu anayeabudu."* (Waebrania 9:9 NEN).
- ✓ Wanadamu wamebuni njia nyingi potofu za kujaribu kukabiliana na dhambi, k.m. kumutoroka Mungu, kulaumu wengine, kupinga, kurazinisha, kujiadhibu, kukata tamaa, n.k.
- ✓ Jibu la kawaida kwa dhamiri ya dhambi ni kujaribu kufidia dhambi kwa kufanya kazi. Hizi ni kazi zilizokufa.
- ✓ Jibu la Mungu kwa dhamiri yenye dhambi ni kupata haki kupitia damu ya Yesu: "B*asi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na dosari, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?"* (Waebrania 9:14).
- ✓ Kuelewa tunavyopata haki yetu kwa njia ya imani katika Kristo ni muhimu kwa uhusiano mzuri na Mungu.
- ✓ Wale wasio na ujuzi katika neno la haki wanaitwa "watoto wachanga". (Tazama Waebrania 5:13). Hatua ya kwanza katika ukuaji wetu wa Kikristo ni kujua kwamba dhambi zetu zote zimesamehewa. Kisha sisi si watoto wachanga tena bali watoto wadogo, (Tazama 1 Yohana 2:12a).
- ✓ Tunahimizwa kuufikia "utimilifu" kwa kutubu kazi zisizo na uhai na kuweka imani katika damu ya Yesu. *"Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu.* (Waebrania 6:1).
- ✓ Neno "utimilifu" lina maana ya kufanya kitu kikamilike ili kutimiza kusudi la kuumbwa kwake. Tuliumbwa kwa ajili ya urafiki na Mungu.

Ili sisi kuwa katika hali hii ya utimilifu, ni muhimu:

A) Tusadiki kwamba Mungu hatambui tena dhambi zetu.

B) Tusitambue tena dhambi zetu, bali tuwe na utambuzi mkubwa sana kuwa sisi ni wenyehaki.


**A) <u>Mungu Hatambui Tena Dhambi Zetu</u>**

- ✓ Agano jipya ni agano lililo bora zaidi linalotegemea ahadi zilizo bora zaidi, (Tazama Webrania 8:6&7).
- ✓ Mojawapo ya ahadi hizo bora zaidi ni kwamba kupitia kifo cha Yesu dhambi zetu zimeondolewa kabisa na milele machoni na mawazoni mwa Mungu. *"Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, Na dhambi zao sitazikumbuka tena."* (Waebrania 8:12).
- ✓ Sio tu kwamba Mungu hatakumbuka dhambi zetu tena, bali pia mbingu zimetakaswa *rekodi* ya dhambi zetu, (Tazama Waebrania 9:23-26).
- ✓ Kwa muumini, Ujio wa Pili wa Yesu hautakuwa na marejeleo yoyote ya dhambi: *"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu; kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu."* (Waebrania 9:27&28).
- ✓ Mungu hatamhukumu muumini kamwe.

**B) <u>Tusitambue Tena Dhambi Zetu, Bali Haki Yetu</u>**

- ✓ Dhamiri zetu zinazungumza nasi kuhusu hali yetu ya kiadili.
- ✓ Lakini zinaweza tu kuripoti kwa usahihi ikiwa zimefahamishwa kwa usahihi.
- ✓ Kazi ya dhamiri ni kuzungumza na<u>si</u>; lakini kazi ya damu ni kusema naye <u>Mungu</u>. "*Bali ninyi mmeufikia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika, na Yesu mjumbe wa agano jipya, <u>na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili</u>"* (Waebrania 12:22-24).

- ✓ Dhamiri yetu inaweza kuwa dhaifu na kupotoshwa, lakini Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu. *"...ikiwa mioyo yetu inatuhukumu; kwa maana Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua yote."* (1 Yohana 3:20).
- ✓ Shetani ndiye mshitaki wa ndugu. Anatumia dini kwa ajili hiyo. Dini inatukumbusha dhambi. Tunaona hili katika utoaji wa daima wa dhabihu chini ya agano la kale. Kwa desturi hii ya kurudia-rudia, kulikuwamo ukumbusho wa mara kwa mara wa dhambi.
- ✓ *"Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wowote kuwakamilisha wakaribiao. Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi? Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka."* (Waebrania 10:1-3).
- ✓ Tatizo hilo hilo lipo, Ukristo unapozingatia dhambi.
- ✓ Dini inakumbusha; lakini Mungu husahau. Wokovu wake haukabili dhambi tu, bali pia dhamiri yenye dhambi. "*Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kulia wa Mungu; Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa."* (Waebrania 10:12&14).
- ✓ Roho Mtakatifu hatushawishi kuhusu dhambi, bali kuhusu haki, *"Na Roho Mtakatifu naye amshuhudia; kwa maana, baada ya kusema, 'Hili ni agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana, Nitatia sheria zangu mioyoni mwao, Na katika fikira zao nitaziandika; ndipo anenapo, Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa."* (Waebrania 10:15-17).
- ✓ Yeye ndiye Mfariji. "*Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu."* (Warumi 8:15&16).
- ✓ Roho Mtakatifu ametolewa kwetu ili kutuonyesha mambo ambayo tumepewa bure katika Kristo, (Tazama 1 Wakorintho 2:9-12).



**Kwa Majadiliano**

1. Tangu ulipokuwa Mkristo umepambana na hatia? Ulikabilianaje nayo?

2. Mpaka tutakapokuwa na ujuzi katika mafundisho ya haki kwa njia ya imani katika Kristo itakuwa vigumu kukua katika maisha ya Kikristo. Je, huu umekuwa ujuzi wako wakati wowote? Ni lini na jinsi gani ufunuo wa haki ulikuja kwako?

3. Je, sasa unasadiki kwamba Mungu hatambui tena dhambi zako? Je, unaamini kwamba Yesu atakapokuja tena hatarejelea kabisa dhambi zako?

4. Ni kwa njia gani dhamiri yetu inaweza kupotoshwa, na hivyo kusababisha tuwe na dhamiri ya dhambi?

5. Je, unaamini kwamba ni lazima kuungama dhambi zako kabla ya kusamehewa?

6. Ni kwa njia gani umeelewa jukumu la Roho Mtakatifu - kama Yule anayewahukumu Wakristo kuhusu dhambi, au kama Yule anayewafariji kuhusu haki yao na hadhi yao kama wana wa Mungu?

# Somo #5 - Neema

*"... Wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo."* (Warumi 5:17).

Neema ni njia ambayo Mungu anahusiana nasi chini ya agano jipya. Shetani anatumia dini kama jaribio la kubadilisha neema na uhalali.

- ✓ Uhalali ni imani kwamba kazi zangu ndio msingi wa kukubalika na kupata baraka za Mungu. Mkazo ni binafsi.
- ✓ Neema ni imani kwamba ninakubalika kila wakati na kustahili kwa kila baraka kwa sababu ya kazi iliyokamilika ya Yesu. Mkazo ni Yesu.

**Uhalali**

- ✓ Uhalali unavuta kinyume na Msalaba. Unajaribu kutufanya tulipie kile ambacho Mungu amekwisha kulipa. Unatumia torati kwa kusudi hili.
- ✓ Biblia inatumia neno 'Torati' kwa kurejelea sheria ya Musa. Lakini inapotumia neno 'sheria' inataja mfumo wowote wa kisheria tunaoweza kutumia ili kupata kibali cha Mungu, au ambao kwao tunaweza kujaribu kubadilika.
- ✓ Warumi 7:1-4. Agano Jipya halipingani na Torati, bali linapinga sisi kuolewa na Torati. Kupitia muungano wetu na Kristo tumeifia Torati ili tupate kuolewa na Kristo. Sasa yeye ndiye chanzo cha utakatifu wetu. Katika Kristo hatuna Torati, bali uzima.

**Dhana Potofu Kuhusu Torati Na Neema**

1) 'Torati itanisaidia kuishi maisha bora'
   - ✓ Paulo alidanganywa na kuamini hivyo, *"Kwa maana dhambi, kwa kupata nafasi kwa ile amri, ilinidanganya, na kwa hiyo ikaniua"* (Warumi.7:11).
   - ✓ Torati hutuchochea kutenda dhambi, wala si kuishi kwa utakatifu, *"Kwa maana tulipokuwa katika hali ya mwili, tamaa za dhambi, zilizokuwako kwa sababu ya torati, zilitenda kazi katika viungo vyetu hata mkaizalia mauti mazao"* (Warumi.7:5);

   *"Lakini dhambi ilipata nafasi kwa ile amri, ikafanya ndani yangu kila*

*namna ya kutamani. Kwa maana dhambi bila sheria imekufa.’* (Warumi.7:8)

- ✓ Sheria ni dhaifu kwa sababu msingi wa matumizi yake ni mwili. “*Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili.”* (Warumi.8:3).
- ✓ Wanauhalali wana nia ya kufanya yaliyo sahihi, lakini hawana uwezo. “*Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema siwezi.”* (Warumi.7:18).

2) ‘<u>Ninaamini katika neema; lakini lazima isawazishewe na sheria</u>'

- ✓ Tunachoita ‘usawa’ Mungu anaita ‘mchanganyiko’. “*Lakini ikiwa ni kwa neema, haiwi kwa matendo tena, au hapo neema isingekuwa neema. Lakini ikiwa ni kwa matendo, haiwi kwa neema tena; au matendo si matendo tena”* (Warumi 11:6).
- ✓ Ili neema ifanye kazi lazima ibaki kuwa kali. Injili ya neema kama ilivyofundishwa na Paulo ni, “... *uweza wa Mungu uletao wokovu.”* (Warumi.1:16). Tukiirudia torati kama njia ya kuishi, Kristo ataacha kuwa na athari yoyote maishani mwetu, (Tazama Wagalatia 5:4).

3) ‘<u>Neema ni ruhusa tu ya kutenda dhambi</u>'

- ✓ Neema kamwe haiwahimii watu kutenda dhambi, “*Maana neema ya Mungu iwaokoao wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na kufunuliwa kwa utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wake mwenyewe walio na bidii katika matendo mema.”* (Tito 2:11-14 ).
- ✓ Neema ndicho kitu pekee kinachoweza kututoa katika dhambi. “*Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema.”* (Warumi 6:14).

4) ‘<u>Ninaamini katika neema, lakini bado tunapaswa kufanya sehemu yetu</u>'


- ✓ Sehemu yetu ni kuamini kwamba Yeye amefanya yote." *Yesu akajibu, akawaambia, Hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini yeye aliyetumwa na yeye."* (Yohana 6:29).
- ✓ Wenye haki wanaishi kwa imani. "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."* (Wagalatia 2:20).

5) '<u>Ukitaka baraka za Mungu, kuna gharama ya kulipa</u>'

- ✓ Tayari tumebarikiwa na vitu vyote. "*Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo."* (Waefeso 1:3). Tunapopokea zawadi ya haki, tunastahili kwa kila jambo jema. "*Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa."* (Mathayo 6:33).
- ✓ Bei tayari imelipwa kikamilifu. Mambo yote tumepewa bure, kwa ajili ya Yesu. "*Ikiwa Mungu hakumhurumia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote <u>kwa ukarimu</u> pamoja naye?"* (Warumi 8:32).

6) '<u>Kwa neema hakuna nia ya kutoa, kutumikia na kutii</u>'

- ✓ Neema inafichua nia yoyote ya biashara katika maisha ya Kikristo.
- ✓ Lakini haitufanyi kuwa wavivu. Kwa kweli inatuwezesha kufanya mengi zaidi kuliko tunayoweza kufanya katika uwezo wetu wenyewe. "*Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nilizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami."* (1 Wokorintho 15:10).



**Kwa Majadiliano**

1. Jadili fafanuzi za 'uhalali' na 'neema' zilizotolewa katika somo hili.

2. Ni zipi baadhi ya amri zilizotungwa na mwanadamu ambazo umetii katika siku za nyuma, ambazo zilikutia chini ya nguvu ya uhalali.

3. Wanauhalali ni watu waaminifu. Wanataka kumpendeza Mungu na wanaamini kwamba njia wanayoitumia ni sahihi. Lakini uhalali wao unaongoza kwenye kazi zilizo kufa na kushindwa. Je, mtazamo wetu unapaswa kuwaje kwa uhalali?

4. Kwa nini uhalali ni hatari katika maisha ya Kikristo?

5. Pingamizi la kawaida kwa mafundisho ya neema ni kwamba ni kibali tu cha kufanya dhambi. Je, ungepingaje kauli hiyo?

6. Ukristo wa biashara ni nini na neema hutuwekaje huru kutoka kwao?

7. Je, neema imekufanya kuwa mzembe katika kumuishia Kristo na kumtumikia?

# Somo # 6 - Imani

*"Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Mgiriki pia. 17 Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hadi imani; kama ilivyoandikwa, Mwenye haki ataishi kwa imani."* (Warumi.1:16-17).

Injili inadhihirisha haki itokayo imani hadi imani. Mafundisho yoyote ya haki itokayo imani hadi matendo ni injili potofu.

**1) Imani Ni Mshirika Wa Neema**

- ✓ Jibu la mwanadamu kwa Mungu chini ya Torati lilikuwa kazi; mwitikio wetu chini ya neema ni imani. Yohana 6:29.
- ✓ Neema ni kile ambacho Mungu ametufanyia; imani ni njia ya kushiriki yale aliyofanya.
- ✓ Imani ni mwitikio wetu kwa yale Mungu ametuandalia katika Kristo.
- ✓ *"...tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake."* (Warumi.5:2).
- ✓ Imani haituokoi. Yesu ndiye anatuokoa; imani hutuwezesha kumpata Yeye.
- ✓ Ni kwa neema tunaokolewa, kwa njia ya imani. Lakini hata imani yetu ni zawadi kutoka kwa Mungu.
- ✓ Kama vile tulivyompokea Kristo kwa imani, ndivyo tunavyoishi kwa imani.
- ✓ Paulo aliwakemea Wagalatia kwa sababu walikuwa wamedanganywa kutoka kwa imani na kurejea matendo ili kupata haki. Akawauliza, *"Je! Mmekuwa wajinga namna hii? Baada ya kuanza katika Roho, mnataka kukamilishwa sasa katika mwili?"* (Wagalatia 3:3).
- ✓ Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu. Chochote ambacho si cha imani ni dhambi.


**2) Kristo Ndiye Lengo Kuu La Imani Yetu.**

- ✓ Watu hujaribu kuishi kwa imani katika imani yao. Lakini imani lazima iwe na kitu cha kutumainia.
- ✓ *Kwamba* unaamini sio suala; *Ni nini* unaamini, ndilo swala.

- ✓ Nguvu ya imani yetu inaamuliwa na nguvu ya kitu tunachokiamini.
- ✓ Lengo kuu la imani yetu ni Kristo.
- ✓ Katika Agano lote la Kale, ambalo ni takriban 75%-80% ya Biblia, imani imetajwa mara 15 tu. Sababu ni kwamba lengo kuu la imani yetu, Yesu Kristo, alikuwa bado halijafika. *"Lakini andiko limeyafunga yote chini ya nguvu ya dhambi, makusudi hao waaminio wapewe ile ahadi kwa imani ya Yesu Kristo. Lakini kabla ya kuja ile imani tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ije ile imani itakayofunuliwa."* (Wagalatia 3:22-23).
- ✓ Takriban aya 115 katika Agano Jipya zinafundisha kwamba wakati mtu *anamuamini* Kristo (kitenzi), anaokolewa, ana uzima wa milele, anahesabiwa haki, n.k. Zaidi ya hayo kuna takriban mistari 35 inayosema kwamba mtu anaokolewa, anahesabiwa haki au anakuwa mwenye haki kwa njia ya *imani* (nomino). Kwa ujumla takriban mara 150 imani pekee inawasilishwa kama mwitikio wetu kwa neema ya Mungu.
- ✓ Katika kila moja ya aya hizi hakuna sharti lingine linalodaiwa. Hakuna kitu kinachochanganywa au kuongezwa kwa imani kama sharti la wokovu.
- ✓ Imani yetu sio katika Biblia, bali katika Kristo. Biblia ni ufunuo wa Mungu kumhusu.
- ✓ Tunaweza kuijua Biblia lakini tusimjue Kristo, kama walivyofanya Mafarisayo. Yesu akawaambia, *"Mnayachunguza maandiko kwa sababu mnadhani kuwa ndani yake ninyi mna uzima wa milele; na maandiko yayo hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima."* (Yohana 5:39-40). Kama kwa kweli waliielewa Biblia, wangemjua Yeye. Tazama Yohana 5:46-47.
- ✓ Imani ya kweli ya kibiblia inamtazama Kristo. Kuyaacha yote na kumwaamini Yesu.
- ✓ Wale walio na imani, wanamthamini Kristo sana. *"Kwenu ninyi mnaoamini, jiwe hili ni la thamani..."* (1 Petro 2:7).
- ✓ Ili kuongeza imani yako kwa Mungu lazima uongeze maarifa yako kumhusu, aliye lengo la imani yetu.

3) **Shukrani Ni Lugha Ya Imani**

- ✓ Kunung'unika na kulalamika ni lugha ya kutoamini; kushukuru ni lugha ya imani.
- ✓ Tunadhihirisha imani yetu kwa kumshukuru Mungu kwa kazi iliyokamilika ya Kristo, ambayo hutufanya kuwa wakamilifu na watimilifu kwa mambo yote.
- ✓ "*Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu <u>dhabihu ya sifa</u> daima, yaani, tunda la midomo iliungamalo jina lake.*" (Waebrania 13:15).
- ✓ Yesu alionyesha imani yake kwa Baba kwa kutoa shukrani.
- ✓ Kwa mfano, katika kulisha watu 5,000. "*Basi Yesu akaitwaa ile mikate, <u>akashukuru</u>, akawagawia walioketi; na kadhalika katika wale samaki kwa kadiri walivyotaka.*" (Yohana 6:11). "*...lakini zikaja mashua nyingine kutoka Tiberia mpaka karibu na mahali pale walipokula mikate, wakati Bwana <u>aliposhukuru</u>.*" (Yohana 6:23).
- ✓ Pia, katika kufufuka kwa Lazaro. "*Basi wakaliondoa lile jiwe. Yesu akainua macho yake juu, akasema, Baba, <u>nakushukuru</u> kwa kuwa umenisikia.*" (Yohana 11:41).
- ✓ Katika hali zote mbili Yesu alitoa ushahidi wa imani yake katika udhibiti wa Baba juu ya mazingira.
- ✓ Tunadhihirisha imani yetu mfululizo kwa njia iyo hiyo. "*...shukuruni kwa kila jambo...*" (1 Wathesalonike 5:18).
- ✓ Tunatoa shukrani si tu kwa yale aliyofanya bali kwa yale atakayofanya.
- ✓ Ametutosheleza kwa kila kitu. Mungu, ambaye alitupa wokovu katika Kristo, amefanya utoaji wa mahitaji mengine yote ndani yake. Warumi 8:32.
- ✓ *"Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, ishini vivyo hivyo katika yeye; 7 wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi <u>kutoa shukrani</u>."* (Wakolosai 2:6&7).
- ✓ Kwa hiyo, tunapaswa, "*kuomba, <u>pamoja na kushukuru</u>.*" (Wafilipi 4:6) na "*Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba <u>mkiwa na shukrani</u>.*" (Wakolosai 4:2).



**Kwa Majadiliano**

1. Kwa nini haki ya Mungu imefunuliwa katika Injili, "kutoka imani hadi imani"?

2. Jadili njia ambayo imani ni mshirika wa neema.

3. Kwa nini imani ilitajwa mara chache sana katika Agano la Kale, hasa kwa kulinganisha na Agano Jipya?

4. Kwa nini unafikiri kwamba imani inampendeza Mungu sana?

5. Jadili hatari ya kuwa na ujuzi mkubwa wa Biblia ambao hauelekezi kwenye imani ya kila siku katika Kristo.

6. Toa baadhi ya mifano kutoka katika Biblia ambapo:
   a) Manung'uniko yalikuwa lugha ya kutoamini na,
   b) Shukrani ilikuwa lugha ya imani.

7. Unaweza kutoa mfano wa haya kutoka kwa maisha yako mwenyewe?

# Somo # 7 - Agano Jipya

Soma Wagalatia 3:5-9. Mungu ni Mungu wa maagano. Ili kuhusiana Naye kwa usahihi ni lazima tuelewe maagano.

- ✓ Agano la Ahadi ambalo Mungu alifanya na Abrahamu ndilo agano msinigi na kuu katika Biblia.
- ✓ Linahusu mpango wa Mungu wa ukombozi wa dunia nzima na ni sawa na Agano Jipya, linalomhusu Yesu, (3:8).
- ✓ Katika maagano haya yote mawili, haki inapewa wale wanaomwamini Kristo.

Basi mbona Agano la Musa lilihitajika na ni upi uhusiano wake na Agano la Ahadi? Katika Wagalatia 3 Paulo anataja hoja hizi 4:

1) **Agano la Mungu la Ahadi na Abrahamu halibatiliwi, kurekebishwa au kubadilishwa na Sheria, (Wagalatia 3:15-17)**
   - ✓ 3:15. Baada ya kuidhinishwa, agano lisilo na masharti haliwezi kurekebishwa au kubatilishwa na tabia ya mwanadamu.
   - ✓ Mungu peke yake alisimamia Agano la Ahadi na Abrahamu, (Tazama Waebrania 6:13-18). Ni agano lisilo na masharti.
   - ✓ 3:16. Mungu hakuwahi kufanya agano moja kwa moja nasi, au sisi pamoja Naye. Ahadi zilitolewa kwa Abrahamu na Kristo. Tumejumuishwa kwa sababu tuko ndani ya Kristo.
   - ✓ 3:17. Sheria ilikuja miaka 430 baada ya Agano la Ahadi. Haijalishi kusudi lake lilikuwa lipi, haikubatilisha agano la Mungu pamoja na Abrahamu kwa njia yoyote.


2) **Sheria haiwasilishwi kama mbadala wa imani kama njia ya wokovu, (Wagalatia 3:18).**
   - ✓ 3:18. Mungu hakumwokoa Abrahamu kwa sheria bali kupitia imani katika ahadi ya Mungu kuhusu Mzao ajae.
   - ✓ Ikiwa haki ingekuja kupitia Sheria, basi Mungu hangemtuma Mwanawe kufa kwa ajili yetu. *"...kama ingalitolewa sheria iwezayo kuhuisha, hakika haki ingalipatikana kwa sheria."* (Wagalatia 3:21)

3) **Kusudi la Sheria lilikuwa ni kuunga mkono Agano la Ahadi, (Wagalatia 3:19-25)**
   - ✓ 3:19a. Ikiwa sheria haikutupa haki na haitutakasi, kwa nini ilitolewa?
   - ✓ Ilitolewa *'kwa sababu ya makosa,'* ya Waisraeli. Walikuwa na mwelekeo wa kuabudu sanamu. Sheria iliwatia alama kama watu waliotengwa kwa ajili ya Mungu.
   - ✓ Mungu alipowatoa Waisraeli Misri, alifanya nao agano ambalo liliwatawala kitaifa, kistaarabu, kiibada na kimaadili. Hii ndiyo njia pekee ambayo wangeweza kuhifadhiwa kama watu wa pekee walioituliwa kuweka hai ahadi ya Mzao Ajae. Walikuwa *''wamewekwa chini ya sheria"* (3:23).
   - ✓ 3:21-22. Sheria sio adui wa Ahadi. Ilitumikia na kuunga mkono Ahadi.
   - ✓ Ilikuwa ya mpito, ya muda mfupi; si agano la milele, kama wengine wasemavyo, (3:19&25).

4) **Sheria ilielekea kulaaniwa; Ahadi ina sifa ya baraka, (Wagalatia 3:10-14)**
   Tofautisha 3:9 na 10. Chini ya Agano Jipya:
   Tuko huru kutokana na laana kwa sababu Kristo alifanyika laana, yaani "aliyelaaniwa" kwa ajili yetu.
   - ✓ Laana hii ilionyeshwa waziwazi kwa njia ambayo Kristo alikufa. Chini ya sheria, mtu aliyetundikwa juu ya mti alilaaniwa. "*mzoga wake usikae usiku kucha juu ya mti; lazima utamzika siku iyo hiyo; kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu; usije ukatia unajisi katika nchi yako akupayo BWANA, Mungu wako, iwe urithi wako* (Kumbukumbu 21:23).
   - ✓ Yesu alikumbana na laana ya torati hadi akapaza sauti, "Imekwisha." Yaani hadi sheria na laana yake zilipotimia.
   - ✓ Njia pekee ambayo muumini anaweza sasa kuipata laana ni kwa kujaribu kuishi kwa sheria.
   - ✓ 3:13-14. Hatujalaaniwa bali tumebarikiwa, (Tazama pia 3:8&9).
   - ✓ Inatupasa kuwa tunasoma kuhusu baraka, sio laana! K.m. tazama Waefeso 1:3-14; 1 Wakorintho 2:9-12.

**Maagano Ya Kale Na Jipya Yanafasiriwa Katika Fumbo La Sara Na Hajiri, Wagalatia 4:21-31**

- ✓ Waumini wa Kiyahudi walijisifu kwamba walikuwa wana wa Abrahamu, yaani, wazao wa kimwili. Lakini alikuwa na wana wawili, Isaka na Ishmaeli, kutoka kwa mama tofauti. Hadhi ya kila mwana iliamuliwa na hadhi ya mamake. Akawauliza, *"Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini ya sheria, je! Hamwisikii sheria? Kwa maana imeandikwa ya kuwa, Abrahamu alikuwa na wana wawili mmoja kwa mjakazi, na mwingine kwa mwanamke huru.* ( Wagalatia 4:21-22 ).
- ✓ Hawa waliwakilisha maagano mawili ya Ahadi (Sara) na Sheria (Hajiri). "*Mambo haya husemwa kwa mfano; kwa maana hawa ndio kama maagano mawili, moja kutoka mlima Sinai, lizaalo kwa utumwa, ambalo ni Hajiri. Maana Hajiri ni kama mlima Sinai ulioko Arabuni, umelingana na Yerusalemu wa sasa; kwa kuwa yuko utumwani pamoja na watoto wake. Bali Yerusalemu wa juu ni muungwana, naye ndiye mama yetu sisi."* (Wagalatia 4:24-26 ).
- ✓ Paulo anadai, *"Basi, ndugu zangu, kama Isaka sisi tu watoto wa ahadi."* (Wagalatia 4:28).
- ✓ Lakini anawauliza wanatorati, "Mama yenu ni nani?"
- ✓ Sheria na neema haviwezi kuwepo pamoja. Moja lazima iondolewe. Hajiri na Ishmaeli walipofukuzwa, amani ilirejea katika nyumba ya Abrahamu. Tutakapoachana na uhalali ndipo tutajua amani. *"…Lakini lasemaje andiko? Mfukuze mjakazi na mwanawe, kwa maana mwana wa mjakazi hatarithi kabisa pamoja na mwana wa muungwana."*(Wagalatia 4:30).
- ✓ Usijaribu kuchanganya maagano. Usikate kipande cha vazi la agano jipya ili kuweka kiraka katika vazi la agano la kale! Tupa lile vazi kuukuu na uvae lile jipya!
- ✓ Tunapaswa kupigana dhidi ya jaribio lolote la kuingizwa utumwani wa Sheria tena. "*Katika uhuru huo Kristo alituweka huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa."* (Wagalatia 5:1).



**Kwa majadiliano**

1. Ni ufanano upi na ni tofauti ipi iliopo kati ya Agano la Ahadi, ambalo Mungu alifanya na Abrahamu, na Agano Jipya ambalo tumejumuishwa?

2. Je, Agano la Musa ni bora au duni kuliko Agano la Ahadi? Kwa nini?

3. Kulingana na Wagalatia 3:21 na Warumi 10:3 ni kosa gani kubwa ambalo Wayahudi walikuwa na hatia ya kulifanya?

4. Ni kwa njia gani Agano la Musa liliunga mkono Agano la Ahadi?

5. Je, umewahi kukubaliana na mafundisho yasiyo sahihi kuhusu laana? Shiriki ujuzi wako.

6. Orodhesha baadhi ya baraka ambazo sasa ni zetu katika Kristo.

7. Je, umewahi kuchukua hatua madhubuti za 'kumfukuza mjakazi' kutoka kwa maisha yako, k.m. kutupa vitabu, CD's, DVD's zinazofundisha uhalali au mchanganyiko. Je, umewahi kujitenga na watu ambao mafundisho yao yalikuwa na matokeo ya kukurejesha utumwani?

8. Ni kwa njia gani umelazimika kupigana dhidi ya majaribio ya kukurejesha utumwani wa sheria?

# Somo # 8 - Wana wa Mungu

- ✓ Katika kipindi cha agano la kale watu wa Mungu walikuwa chini ya ulinzi wa sheria. Hii inaonyeshwa na desturi ya mtoto kuwa chini ya mlezi (mtumishi wa nyumbani) katika nyakati za Agano Jipya. *“Kabla ya kujaliwa imani, sheria ilitufanya wafungwa, tukingojea imani hiyo ifunuliwe. Basi, hiyo sheria ilikuwa kama mlezi wetu mpaka alipokuja Kristo, ili kwa njia ya imani tufanywe waadilifu mbele yake Mungu."* (Wagalatia 3:23-24).
- ✓ Chini ya mpango huu mtoto hakuwa bora zaidi kuliko mtumishi wa nyumbani. *“Basi, nasema hivi: Mrithi, akiwa bado mtoto, hawi tofauti na mtumwa ingawaje mali yote ni yake. Wakati huo wote yuko chini ya walezi na wadhamini mpaka wakati ule uliowekwa na baba yake.”* (Wagalatia.4:1-2).
- ✓ Lakini kulikuwa na wakati maalum, kwenye sherehe maalum, ambapo haya yalibadilika. Kisha, mtoto aliasiliwa rasmi katika familia ya baba yake. Hakuwa tena ‘mtoto’ bali ‘mwana’.
- ✓ Pale msalabani ulikuwa wakati wa kubainisha ambapo watu wa Mungu walikoma kuwa watumishi tena bali wakawa wana. *“Lakini wakati ule maalumu ulipotimia, Mungu alimtuma Mwanae aliyezaliwa na mwanamke, akaishi chini ya sheria, apate kuwakomboa wale waliokuwa chini ya sheria ili sisi tufanywe wana wa Mungu.”* (Wagalatia 4:4-5).
- ✓ Tukio hili lilikuwa na vipengele hivi:
  1) Uhuru kutoka kwa mkufunzi (sheria)
  *“…imani imekwisha fika, sisi hatuko tena chini ya mlezi"* (Wagalatia 3:25);
  2) Urafiki wa karibu na Baba
  *“Kwa njia ya imani, nyinyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu kwa kuungana na Kristo.”* (Wagalatia 3:26).
- ✓ Yesu alisema, *“Wala mtumwa hakai nyumbani sikuzote; mwana hukaa sikuzote.”* (Yohana 8:35). Mtumishi hutumikia ili kudumisha nafasi yake ndani ya nyumba. Nafasi ya mwana katika nyumba ni salama kwa sababu haitegemei utumishi wake bali hadhi yake kama mwana.

**Tumefia Sheria Na Tunaishi Kwa Roho**

- ✓ Kwa kila muumini Roho Mtakatifu amechukua nafasi ya torati. *"Lakini*

*mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria."* (Wgalatia 5:18). Tumeifia sheria na tunaishi kwa Roho.


- ✓ Katika Wagalatia 4:4 tunasoma kwamba Mungu alimtuma *Mwanawe*; Katika Wagalatia 4:6 tunaambiwa alituma *Roho* wa Mwanawe.
- ✓ Katika Kristo tunayo *hadhi* ya wana; kupitia Roho tunapata *ujuzi w*a wana. Roho hutusaidia kujihisi kama wana, jinsi Yesu Mwenyewe alivyojihisi katika uwepo wa Baba.
- ✓ Haifai kwa wale waliopata hadhi ya kuwa wana wahusiane na Baba kwa misingi ya sheria, amri, kanuni n.k. Hii itakuwa ni kurudi kwenye hali ya utoto/utumishi.
- ✓ Cha kusikitisha ni kwamba, hivi ndivyo Wagalatia walifanya walipoangukia mikononi mwa walimu wa sheria. *"Bali sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, kwa nini kuyarejea tena mafundisho ya kwanza yaliyo manyonge, yenye upungufu, ambayo mnataka kuyatumikia tena? Mnashika siku, na miezi, na nyakati, na miaka. Nawachelea, isiwe labda nimejitaabisha bure kwa ajili yenu."* (Wagalatia.4:9-11).

**Hali Ya Uwana Ina Sifa Ya Ukaribu Na Baba**

- ✓ Dhana ya utumishi haiambatani tu na sheria bali pia utegemezi kwa watoa sheria. Watu wenye fikra za utumishi siku zote wanahitaji mtu wa kuwaambia cha kufanya. Wanahitaji mpatanishi wa kibinadamu kati yao na Mungu.
- ✓ Hadhi ya uwana ina sifa ya ukaribu na Baba.
- ✓ Wana wanaongozwa na Roho. *"Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu."* (Warumi.8:14).
- ✓ Chini ya agano jipya kuna kiwango kipya cha urafiki unaotegemea aina mpya ya uhusiano. Hakuna mpatanishi wa kibinadamu kati yetu na Mungu. "*Nao hawatafundishana kila mtu na jirani yake, Na kila mtu na ndugu yake, akisema, Mjue Bwana; Kwa maana wote watanijua, Tangu mdogo wao hata mkubwa wao."* (Waebrania 8:11).
- ✓ Tukipungukiwa katika ufahamu wa maana ya kuwa wana ndivyo tutazidi kuwa kama watumishi. Tutahitaji sheria, na mtu wa kutuambia nini cha kufanya.
- ✓ Yesu alisema, *"Kondoo wangu huisikia sauti yangu."* Ni lazima tujifunze

kutofautisha sauti yake na sauti ya wageni.

- ✓ Kadiri tunavyoijua tabia yake ndivyo tutakavyoitambua sauti yake.



**Kwa majadiliano**

1. Kwa nini Msalaba ulikuwa wakati wa kubainisha ambapo watu wa Mungu hawakuwa watumishi tena bali wana? Ni mabadiliko gani mengine kwa watu wa Mungu yalifanyika pale Msalabani?

2. Kwa nini ni muhimu kuwa huru kutoka kwa sheria ili kujua na kufurahia ukaribu na Baba?

3. Roho Mtakatifu amechukua nafasi ya sheria katika maisha ya muumini. Jadili nafasi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya Mkristo.

4. Ni mbinu kuu ya Shetani kuwaweka watu wa Mungu chini ya sheria, au kuwarudisha wale walio huru chini yake. Kwa nini iko jinsi hii?

5. Kuwa huru kutokana na hitaji la mpatanishi wa kibinadamu kati yetu na Mungu haimaanishi kwamba hakuna tena nafasi ya wachungaji, walimu, viongozi n.k. katika kanisa. Je, unaweza kuelezaje tofauti kati ya kuwa na uhusiano uliopungukiwa na Mungu kupitia kuwategemea wengine, na kufaidika na huduma ya wachungaji, walimu, n.k.?

6. Je, umejifunzaje kutambua sauti ya Roho Mtakatifu katika maisha yako? Unawezaje kuitofautishaje na hisia zako mwenyewe?

7. Shiriki ujuzi wako wa ukuaji na maendeleo katika ukaribu wako na Baba.

# Somo la 9 - Kiumbe Kipya

Biblia inataja asili yetu mara mbili:

1) Utu wetu wa kale tulioupokea kutoka kwa Adamu wakati wa kuzaliwa, *"Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; ambao zamani, sisi sote nasi tulienda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira, kama wengineo wote."* (Waefeso 2:1-3).

2) Asili yetu mpya tuliyopokea wakati wa kuzaliwa upya. Tulibatizwa katika Kristo na tukawa, "…*washiriki wa asili ya kimungu."* (2 Petro 1:4). *"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama! Yamekuwa mapya."* (2 Wakorintho 5:17).

Hii inamaanisha:

- ✓ Tulifia kile tulichokuwa ndani ya Adamu na sasa tumeunganishwa na Kristo. "*Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye."* (1 Wakorintho 6:17).
- ✓ Kama vile tawi linavyopandikizwa katika mzabibu ndivyo sisi tunapandikizwa katika, "…*Kristo aliye uhai wetu…"* (Wakolosai 3:4).
- ✓ Agano la kale lilikuwa linatoa sheria; agano jipya latoa uhai.
- ✓ Tulikuwa viumbe wa aina moja lakini sasa ni wa aina nyingine. Tulikuwa tumekufa lakini sasa tuko hai. Zamani tulikuwa giza, lakini sasa sisi ni nuru, n.k. (Tazama Waefeso 2:1; 5:8).
- ✓ Kwa kweli kiumbe hiki kipya hakiwezi kufanya dhambi wala hakitaki kutenda dhambi! "*Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki ana haki, kama yeye alivyo na haki; atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi. Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu."* (1 Yohana.3:7-9).

**Lakini Wakristo Bado Wanatenda Dhambi**

Hata hivyo, kama Wakristo tunafanya dhambi. Je, unafanyaje unapotenda dhambi?

Mkristo anapotenda dhambi, mambo mawili yanahitaji kueleweka - utambulisho wetu na tabia zetu.

- ✓ Utambulisho wetu u ndani ya Kristo; ni jinsi tulivyo sasa ndani Yake. Ni jinsi tulivyo katika roho zetu.
- ✓ Mwandishi kwa Waebrania anatufafanua kama, "…*roho za watu wenye haki waliokamilika"* (Waebrania 12:23).
- ✓ Ndani yake sisi ni wakamilifu, hatuna dhambi na hatuharibiki. Roho zetu haziwezi kuharibiwa na dhambi.


- ✓ Tabia zetu hufanyika katika eneo la miili yetu, viungo vyetu. Masalia ya dhambi yanakaa ndani ya miili yetu ambayo haijakombolewa. Bado tunaweza kujaribiwa, na tunajaribiwa. Bado tunaweza kutenda dhambi, na wakati mwingine tunatenda.
- ✓ Hili linapotokea roho zetu huchukizwa. Hiyo ni kwa sababu hatuna asili ya dhambi. Tuna asili ya uungu na hii inapinga dhambi. *"Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani, lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka wa ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu."* (Warumi 7:20, 22-23 ).
- ✓ Kwa hiyo Mkristo anapotenda dhambi vita vya wenyewe kwa wenyewe hutokea ndani yake. Mwili hupigana na Roho na Roho dhidi ya mwili.

**Angalia Kwenye Kioo Ili Kuona Ukweli Kuhusu Jinsi Ulivyo!**

- ✓ Katikati ya vita hivi vya wenyewe kwa wenyewe Shetani anajaribu kutufanya tujenge utambulisho wetu juu ya tabia zetu.
- ✓ Ni lazima tuwe wazi kuhusu tofauti kati ya tabia zetu ambazo hufanyika katika eneo la mwili na utambulisho wetu ambao ni jinsi tulivyo katika Roho. "*Na Kristo akiwa ndani yenu, mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi; bali roho yenu i hai, kwa sababu ya haki."* (Warumi.8:10).
- ✓ Tutasuluhisha mkanganyiko huu kwa kutazama Neno la Mungu badala ya

tabia zetu.

- ✓ Kama vile kioo huakisi kwa usahihi ukweli kuhusu sura yetu, ndivyo Neno la Mungu hufunua yaliyo ya kweli kutuhusu sasa tukiwa viumbe vipya.
- ✓ *"Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo."* (Yakobo 1:23-24).
- ✓ Yakobo anazungumza hapa kuhusu mtu ambaye anaona ni vigumu kuishi inapaswavyo kwa sababu amejisahau yeye ni nani.
- ✓ Tabia zetu hazitufafanui. Alichokifanya Yesu pale msalabani ndicho kinachotufafanua.
- ✓ Tunapoutazama utukufu wa hadhi yetu ndani ya Kristo kwenye kioo cha Neno la Mungu tabia zetu zinabadilika kuwa sawa na hadhi iyo hiyo.
- ✓ Kile ambacho ni kweli katika roho zetu hatimaye kitajidhihirisha katika jinsi tunavyoishi. "*Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho."* (2 Wakorintho 3:18).
- ✓ Hatuwezi kuwa tunavyostahili hadi tujue sisi ni nani.



**Kwa majadiliano**

1. Tulipookoka tulifia tulichokuwa na pia asili yetu ya kale. Tulizaliwa mara ya pili kama washirika wa asili ya uungu. Wengine hufundisha kwamba sasa tuna asili mbili - asili yetu ya zamani na asili yetu mpya. Je, una maoni gani kuhusu hilo? Je, unafikiri tuna asili mbili, au asili moja tu mpya?

2. Kabla ya kipindi hiki ulihisije kuhusu kauli ya Yohana kwamba Mkristo hatendi na hawezi kutenda dhambi, (1 Yohana 3:7&9)?

3. Je, unafanyaje unapotenda dhambi?

4. Jadili kile unachoelewa sasa kuhusu tofauti kati ya tabia na utambulisho.

5. Katika siku za nyuma, umekuwa na mwelekeo wa kutegemea nini ili kupata ukweli kuhusu utambulisho wako - tabia yako au kioo cha Neno la Mungu?

6. Je, ungejibuje wale wanaosema kwamba mafundisho haya yatawahimiza tu watu kupuuza tabia zao na kutenda dhambi zaidi?

7. Jadili kauli hii: Itakuwa vigumu kwa mtu kuishi jinsi impasavyo ikiwa amejisahau yeye ni nani.

# Somo # 10 - Mtu Mpya

- ✓ Paulo aliwahimiza Waefeso kwamba,"*...mwenende kama inavyostahili wito wenu mlioitiwa."* (Waefeso 4:1).
- ✓ Na aliwaandikia Wafilipi, *"...mwenende kama ipasavyo Injili ya Kristo,.."* (Wafilipi 1:27).
- ✓ Neno *"ipasavyo"* lina maana 'kama inavyofaa au invavyostahili'.

Kuna utekelezaji wa neema ya Mungu kimatendo katika maisha yetu ya kila siku. Cha kusikitisha, kuna mafundisho mengi yasiyo sahihi kuhusu hili.

Kwa mfano:

- ✓ Baadhi hufundisha **upungufu**, yaani, sababu ya kuhangaika katika safari yetu ya Kikristo ni kwamba Mungu ametuacha bila rasilimali za kutosha. Tunahitaji zaidi! Hili huleta mgawanyiko katika mwili wa Kristo kati ya 'walionavyo' na 'wasiokuwa navyo', na husababisha utegemezi wa kiroho ambapo 'walionavyo' huhitaji kuwapokeza 'wasio navyo'. Lakini tayari tuna kila kitu tunachohitaji kwa maisha na utauwa. Ukuaji ni upanuzi tu wa maisha tulionayo tayari.

- ✓ Baadhi hufundisha **uhalali**, yaani, utakatifu hupatikana kwa bidii yetu, au unatokana na kazi zetu. Huu ni urekebishaji wa tabia. Wanaamini kuwa tunaweza kufundisha mwili jinsi ya kuishi vizuri. Lakini, sisi tayari ni watakatifu. Utauwa ni bubujiko la kile ambacho tayari tunamiliki.

- ✓ Baadhi hufundisha **uzembe**, yaani, 'yaache tu, mwachie Mungu!' Wanaofundisha hivyo wanaogopa kwamba aina yoyote ya mawaidha au maagizo kuhusu kuishi kivitendo yataelekeza kwenye kufuata sheria. Lakini aina hii ya ufundishaji inapunguza nguvu. Barua za Paulo zimejaa mawaidha kuhusu jinsi tunavyopaswa kuishi, kwa sababu alijua kwamba tayari tumepewa uwezo wa kuishi kama watoto wa nuru.

Kwa hiyo Paulo alifundisha nini? Mafundisho ya Paulo yako katika sehemu mbili tofauti: *mafundisho*
Na *mawaidha*. Hii ni kama mabapa ya mkasi.


1) **Bapa la kwanza: Mafundisho**

- ✓ A) Kile Kristo *amefanya* kwa ajili yetu, yaani, ametufanya wenye haki, wakamilifu, watakatifu, wana wa Mungu, n.k. Hii inahusu utambulisho wetu katika Kristo kwa njia ya ubatizo katika kifo chake, kuzikwa na kufufuka kwake.
- ✓ B) Kile Kristo *ametupa,* yaani maisha yake ndani yetu. Kila kitu tunachohitaji kwa utauwa huishi ndani yetu. *"Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe."* (2 Petro 1:3). Hivyo, chochote Mungu anachotudai Yeye tayari ametupa.

2) **Bapa la pili: Mawaidha**

- ✓ Tumeitwa kujivika Bwana Yesu Kristo, yaani, kuishi kulingana na hadhi yetu na kuonyesha kile tulicho nacho sasa.
- ✓ *"Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu,"* (Wakolosai 3:12).
- ✓ Tunapaswa kufanyisha kazi kile alichofanya ndani yetu, *"...Fanyeni kazi kwa hofu na tetemeko kwa ajili ya ukombozi wenu, kwani Mungu ndiye afanyaye kazi daima ndani yenu, na kuwapeni uwezo wa kutaka na kutekeleza mambo yanayopatana na mpango wake mwenyewe"* (Wafilipi 2:12-13 SCLDC). Tazama kwamba Paulo anatuambia *tuufanyishe* kazi wokovu wetu, wala sio *tuufanyie* kazi au *tuutumikie*.
- ✓ Tunafanya hivi kwa imani. "*...uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*" (Wagalatia 2:20). Maisha ya Kikristo ni, *"...toka imani hadi imani; kama ilivyoandikwa, Mwenye haki ataishi kwa imani.*" (Warumi 1:17).
- ✓ Tunapomvaa Bwana Yesu Kristo kwa imani, hatutazamii kuupa mwili nafasi. *"Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake."* (Warumi 13:14).
- ✓ Tunapovaa utu mpya katika Kristo, tunavua tabia ya kale, (Tazama Waefeso 4:22-32).

- ✓ Lengo letu si kukabiliana na mwili, bali kutembea katika Roho. Tukienenda kwa Roho matokeo yatakuwa kwamba hatutatimiza tamaa za mwili. "*Basi nasema, Nendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.*" (Wagalatia 5:16).
- ✓ Vivyo hivyo, tukitoa viungo vya miili yetu kwa haki havitapatikana kwa ajili ya kutumikia dhambi (Tazama Warumi 6:13,16,19).
- ✓ Utiifu wetu unawezeshwa na Roho Mtakatifu. *"Kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyaua matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi"* (Warumi 8:13).



**Kwa Majadiliano**

1. Je, umepitia mafundisho yoyote yaliyotajwa hapo juu ambayo yanaelezea safari ya Mkristo kimakosa, k.m. upungufu, uhalali na uzembe? Ikiwa ndivyo, shiriki uliyoyapitia.

2. Katika ulinganisho, ambapo jinsi Paulo anavyofunza inafananishwa na mkasi, kwa nini ni muhimu kwamba 'bapa' la kwanza liwe mafundisho?

3. Zungumzia usemi huu: "Kila kitu unachohitaji kwa ajili ya utauwa hukaa ndani yako." Je, unaweza kuunga mkono usemi huu ukitumia Biblia?

4. Kwa nini ni afadhali kusisitiza 'kuvaa utu mpya', badala ya 'kuvua utu wa kale'? Kwa maneno mengine, kwa nini Paulo anasema tunapaswa kutembea katika Roho, badala ya kusisitiza kwamba tunapaswa kuepuka kutimiza matendo ya mwili?

5. Umepata jambo gani la manufaa zaidi katika somo hili?

# Somo # 11 - Upendo wa Mungu

- ✓ *Kwamba* unaamini Mungu sio muhimu, ila ni *unachoamini* kumhusu.
- ✓ *Unachoamini* kuhusu Mungu huamua jinsi utakavyohusiana Naye.
- ✓ Ukiamini kuwa yuko kinyume nawe na anataka kukuhukumu na kukuadhibu kwa makosa yako, utamwogopa badala ya kumwamini; utamkimbia badala ya kumkaribia.
- ✓ Hofu ina mateso lakini pendo kamili huitupa nje hofu.
- ✓ Upendo wa Mungu ndio msingi wetu wa imani.
- ✓ Hakuna tunachoweza kufanya ili kumfanya Mungu atupende zaidi, wala hakuna tunachoweza kufanya ambacho kitafanya upendo wake upunguke. Tunahitaji ufunuo huu.
- ✓ Mungu anataka tuamke kila siku tukiwa na hisia nzito sana za upendo wake kwetu.
- ✓ Upendo wa Mungu ndio mahali petu pa kupumzikia ... na kwake. *"Mwenyezi-Mungu, Mungu wako yu pamoja nawe yeye ni shujaa anayekuletea ushindi. Yeye atakufurahia kwa furaha kuu, kwa upendo wake atakujalia uhai mpya. Atakufurahia kwa wimbo wa sauti kubwa."* (Sefania 3:17). Atatufanya tupumzike kwa sababu ya upendo wake.

Je, tunapata wapi mtazamo wetu kuhusu Mungu? Yesu ni "*…mfano wa Mungu asiyeonekana…"* (Wakolosai 1:15). Kwa hiyo, sura yoyote tuliyo nayo ya Mungu ambayo hailingani na sura tunayoiona kwa Yesu ni uwakilishi wa uongo wa Mungu.

Uhusiano ambao Yesu alikuwa nao na wanafunzi wake ni kielelezo cha uhusiano ambao Mungu anataka tuwe nao pamoja naye.

- ✓ Yesu aliwapenda wanafunzi wake *'hadi mwisho'* (Yohana 13:1). Neno la Kigiriki la '*hadi mwisho'* ni *telos*, maana yake 'kwa kiwango cha juu kabisa'; 'bila mipaka'. Tafsiri moja inasema, "*Aliwaonyesha kiwango kamili cha upendo Wake."*
- ✓ Je! ni kiasi gani kamili cha upendo Wake?
- ✓ Msalaba ni kiwango kamili cha upendo wa Mungu kwetu. Hakuna

upendo mkuu kuliko huu. *"Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake."* ( Yohana 15:13 ).

- ✓ Yesu alitaka waone kwamba kama vile alivyowapenda wanafunzi, Baba aliwapenda wao pia. *"Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba; tangu sasa mnamjua, tena mmemwona. Filipo akamwambia, Bwana, utuoneshe Baba, yatutosha. Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuoneshe Baba?"* (Yohana 14:7-9).

**Je, Wanafunzi Walipata Ufunuo Wa Upendo Wake?**

- ✓ Wengine waliupata. K.m. Yohana alijitaja mara kadhaa kuwa 'mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda' (Yohana 13:23). Tazama pia Wagalatia 2:20.
- ✓ Baadhi walielekea kuupata. K.m. Petro alifikiri kwamba uhusiano wake na Yesu uliamuliwa na jinsi alivyompenda Yesu. Alitaka kumwonyesha Yesu kwamba anampenda kuliko wanafunzi wengine. Upendo wa Petro uliposhindwa, Yesu alimfunulia kwamba uhusiano wake ulitegemea jinsi Yesu alivyompenda, wala si vinginevyo. (Yohana 13:36-38; 21:15-17).
- ✓ Wengine hawakuupata kamwe. K.m. Yuda. Alikuwa ni mfuasi pekee ambaye hakuishi hata kuuona msalaba, (Yohana 13:24-26).


**Yohana Alipokea Ufunuo Mkuu Zaidi Wa Upendo Wa Mungu Na Alikuwa Mwalimu Bora Zaidi Wa Ufunuo Huo. Alitufundisha Kwamba:**

1) <u>Upendo wa Mungu usio na masharti ndio msingi wa uhusiano wetu na Yeye</u>. *"Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu.* (1 Yohana 4:10).
    - ✓ Tumekita mizizi na kutia msingi katika upendo. Paulo aliomba kwamba kanisa liwe, "*…na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.* (Waefeso 3:17).

- ✓ Mariamu aliketi miguuni pake mpaka alipojua kwamba anapendwa. Kutokana na hili kulitiririka huduma yake kwa Yesu.

2) *Kujua* Upendo wa Mungu hakutoshi; lazima pia *tuliamini*. *“Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake.”* (1 Yohana 4:16 ).
   - ✓ Tunapoamini kwa kweli upendo wa Mungu tunaupata katika hisia zetu. “…*pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.”* (Warumi 5:5).
   - ✓ Ikiwa hatuhisi upendo wa Mungu mioyoni mwetu itakuwa vigumu kuuhifadhi katika mawazo yetu.

3) Imani hufikia ukomavu kupitia ufunuo wa upendo wa Mungu. “…*mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo.”* (1 Yohana 4:18 ).
   - ✓ Hofu haimo katika asili ya Mungu. Haogopi chochote. Kwa hiyo, utakatifu wake, kama sifa zake nyingine zote, si zao la hofu bali upendo.
   - ✓ Vivyo hivyo, woga hautawahi kuzaa utakatifu ndani yetu. Mapenzi tu ndiyo yatakayozalisha. Hofu haitatubadilisha, lakini kuitikia upendo wa Mungu kutatubadilisha zaidi kuliko kitu kingine chochote.
   - ✓ Kwa hiyo, kabla Mungu hajatubadilisha, ni lazima aondoe woga wetu na atufundishe ajabu ya kuishi katika upendo wake. *“… pendo lililo kamili huitupa nje hofu.”* (1 Yohana 4:18).
   - ✓ Hakuna kitu muhimu zaidi kwa ukuaji wa kiroho kuliko kufanya mabadiliko kutoka kwa kuishi kwa hofu hadi kujua upendo wa Mungu na kuitikia.



**Kwa majadiliano**

1. 'Tunakuwa kama Mungu tunayemwamini.' Toa mifano mibaya na mizuri ya hili.

2. Katika injili za Mathayo, Marko, Luka na Yohana tunaona jinsi Mungu alivyo, tunapotazama maisha mazuri ya Yesu - Mungu akidhihirishwa katika mwili. Shiriki baadhi ya ufunuo wa upendo wa Mungu ambao umepokea kutoka kwa vitabu vivi vinne vya injili.

3. Ni picha gani potofu ambazo zimemwakilisha Mungu vibaya hapo awali, na hilo liliathirije uhusiano wako Naye?

4. Jadili 1 Yohana 4:10: *"Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu."*

5. Hisia zetu zina sehemu gani katika kupokea na kuonyesha upendo wa Mungu?

6. Je, unakubali kwamba upendo wa Mungu una uwezo mkubwa zaidi wa kubadilisha maisha yetu, na kwamba hofu ndiyo kikwazo kikubwa zaidi cha kukua katika uhusiano wetu na Mungu?

# Somo # 12 - Uzima wa Milele

Yesu, kwa kumwaga damu yake, amekwisha, *“…kupata ukombozi wa milele”* kwa ajili yetu, (Waebrania 9:12). Sawa na wana wa Israeli jangwani, Wakristo wanaweza kutangatanga jangwani; lakini hakuna kurudi Misri! Wale ambao Mungu amewaokoa wanaokolewa milele.

Sisi ni salama milele:

**1) Kwa Sababu Ya Baba**

- ✓ Katika sura chache za kwanza za Warumi Mungu anaonyeshwa kama Hakimu wetu. Lakini tunaona kwamba hatuhukumu kwa sababu ametekeleza hukumu kamili kwa ajili ya dhambi zetu juu ya Mwanawe kulingana na haki yake.
- ✓ Kwa sababu hiyo hatutahukumiwa tena kwa ajili ya dhambi, *“Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenituma ana uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.”* ( Yohana 5:24 ).
- ✓ Tumetolewa mahakamani na kuletwa katika familia ya Mungu. Mungu sasa ni Baba yetu, *“Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu.”* (Warumi.8:15-16).
- ✓ Wokovu wetu haukuanza na ‘uamuzi’ wetu wa kumfuata Kristo. Ulianzia zamani za milele hadi wakati ujao wa milele. *“Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza.* (Warumi.8:29-30).
- ✓ Wokovu ni kazi ya Mungu tangu mwanzo hadi mwisho.
- ✓ Hatupaswi kufanya makosa kumfananisha Mungu na sisi wenyewe. Anauliza, *“Je! mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye,*

*na asimwonee huruma mwana wa tumbo lake? Hakika wao wanaweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe."* (Isaya 49:15). Balaamu akasema, *"Mungu si mtu, aseme uongo;*

- ✓ *Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalitimiza* (Hesabu 23:19). Kwa maneno mengine Yeye ni mwaminifu hata wakati sisi sio.
- ✓ Ni lazima tufikiri kulingana na ufunuo wa Biblia; si kulingana na akili za kibinadamu. Hii itatuongoza kwenye hitimisho sahihi.
- ✓ Tazama hitimisho la Paulo katika Warumi 8:31-39.


**2) Kwa Sababu Ya Mwana**

- ✓ Tulipookoka Baba alitukabidhi kwa Kristo kwa ajili ya kutulinda. "*Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala yeyote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe."* (Yohana 6:37).
- ✓ Tumefungwa mara mbili ndani ya Baba na Mwana. *'…uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu."* (Wakolosai 3:3).*' "Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. 29Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu."* ( Yohana 10:28-29 ).
- ✓ Tulipomwamini Yesu tuliunganishwa naye katika kifo, kuzikwa na kufufuka kwake.
- ✓ Sasa tumeunganishwa Naye ili tuwe viungo halisi au sehemu za mwili Wake. "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na kila mmoja wenu akiwa kiungo cha mwili huo."* (1 Wakorintho 12:27).
- ✓ Ndivyo tulivyo salama; sisi tu mwili mmoja naye! Ikiwa tunaweza kuangamia, basi mwili wa Kristo ungekatwa vipande vipande.
- ✓ Katika Warumi 8:1, Paulo anasema kwa mkazo kwamba hakuna hukumu kwa wale walio katika Kristo Yesu. Hii ni kauli kamili. Ina maanisha sio sasa, sio milele, kwa ya hali yoyote ile - kamwe!
- ✓ Ikiwa Mungu alituokoa tulipokuwa adui zake, zaidi mno atatuhifadhi sasa kwamba tumepatanishwa naye! Ikiwa Mungu alitupenda tulipokuwa mbele zake katika hali yetu ya dhambi, je, si anatupenda zaidi sana sasa tukiwa mbele zake ndani ya Kristo aliye uzima wetu! *"Bali Mungu aonesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa*

*kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye. Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake."* (Warumi 5:8-10).

**3) Kwa Sababu Ya Roho Mtakatifu**

- ✓ Tulipookoka pia tulitiwa muhuri na Roho Mtakatifu.
- ✓ Hii inatuhakikishia usalama wetu hadi Yesu atakaporudi ili kutuchukua tuwe pamoja naye. "*Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, Habari Njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa mhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake."* (Waefeso 1:13&14).
- ✓ Muhuri ni uthibitisho wa umiliki. Mungu ameweka muhuri juu yetu ili kuonyesha kwamba sisi ni Wake. Muhuri ni Roho Mtakatifu Mwenyewe.
- ✓ Muhuri pia ni ahadi ya nia, kama vile amana au pete ya uchumba. "*Basi Yeye atufanyaye imara pamoja nanyi katika Kristo, na kututia mafuta, ni Mungu, 22 naye ndiye aliyetutia mhuri akatupa arabuni ya Roho mioyoni mwetu."* (2 Wakorintho 1:21-22 ).
- ✓ Tumetiwa muhuri hadi siku ya ukombozi, yaani, siku ya kurudi kwa Kristo. *"Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa mhuri hata siku ya ukombozi." '*(Waefeso 4:30).



**Kwa majadiliano**

1. Kwa nini unafikiri kwamba wengine huhitimisha kwamba tabia mbaya, kutotii au kurudi nyuma kutasababisha kupoteza wokovu wetu? Je, unaamini kwamba dhambi zetu zinaweza ‘kushinda’ neema ya Mungu?

2. Ikiwa kazi kuu ya Mungu ndani yetu ni kutufanya tumwamini, je, ingewezekana kumwamini Mtu tunayefikiri kwamba siku moja anaweza kutukana?

3. Jadili yafuatayo: ‘Ikiwa tunaweza kupoteza wokovu wetu basi hii ingebatilisha yote ambayo Yesu alifanya pale msalabani’.

4. Je, kuna baadhi ya maandiko ambayo yamekufanya uwe na wasiwasi kwa sababu yanaonekana kupendekeza uwezekano wa kupoteza wokovu wako?

5. Chini ya agano la kale Daudi aliomba, *“Usinitenge na uso wako, Wala roho yako mtakatifu usiniondolee.”* (Zaburi 51:11). Je, ingekuwa sawa kwetu kusali sala kama hiyo katika agano jipya?

6. ‘Ukiokolewa mara moja, Umeokolewa milele’ sio fundisho kavu la Wakristo kubishana. Ni ukweli wa thamani kuhusu upendo wa Mungu wa milele na wenye uaminifu kwetu. Shiriki kile ukweli huu unamaanisha kwako.

## Maelezo ya Kuwasiliana na Ken

Ikiwa ungependa kuwasiliana na Ken au kumwalika ili afundishe kwenye kikundi chako, kanisani au konferensi yako, maelezo ni kama ifuatavyo:

**Posta**: Ken Legg Ministries, P O Box 4185, Elanora, Qld 4221, Australia

**Simu**: +61 407 571938)

**Barua** pepe: ken@kenlegg.com.au